# Swahili ab initio SL

## Overall grade boundaries

### Standard level

| **Grade:** | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mark range:** | 0-13 | 14-26 | 27-41 | 42-56 | 57-69 | 70-81 | 82-100 |

## Standard level internal assessment

### Component grade boundaries

| **Grade:** | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mark range:** | 0-3 | 4-7 | 8-11 | 12-15 | 16-18 | 19-21 | 22-25 |

### Kiwango na ufaafu wa kazi iliyowasilishwa

Kazi zilizowasilishwa na wanafunzi zilikuwa za kiwango mwafaka na za kufaa katika kozi hii. Vichocheo vya picha vilivyowasilishwa vilikuwa vya kuchachawisha na kuchangamsha fikira za wanafunzi na hatimaye kuibusha mazungumzo zaidi. Mada

mbalimbali pia zilihusishwa, Maswali kutoka kwa kazi ya uandishi pia yaliulizwa. Kwa jumla, kazi za wanafunzi ziliafikiana na kiwango hiki cha kozi ya Kiswahili ya wastani.

### Utendaji wa mtahiniwa dhidi ya kila kigezo

Wanafunzi wengi waliweza kudhibiti mazungumzo kutoka mwanzo hadi mwisho. Hawakuonyesha kushindwa kabisa kuzungumza bali walijikakamua na hata pale walipokumbana na changamoto, walidhihirisha ukakamavu wa kujaribu na kuendelea kuzungumza au kujibu maswali. Katika kigezo cha A, wanafunzi wengi waliweza kuwasiliana vyema na iwapo hawakuelewa wengine walisikika wakiuliza ufafanuzi kutoka

kwa mwalimu wao na baada ya kuelewa waliendelea na mazungumzo. Wanafunzi wachache sana walijipata wakiingiza maneno ya Kiingereza ambapo baada ya kugundua,

waliweza kurudia kuzungumza Kiswahili. Katika kigezo cha B, wanafunzi walionyesha kufahamu na kuendelea na mawasiliano vilivyo.

### Mapendekezo na mwongozo wa kufundisha watahiniwa wa siku sijazo

Ningependekeza kwamba wanafunzi waweze kusisitiziwa matamshi bora ya lugha ya Kiswahili. Mada na miktadha ya utamaduni wa Kiswahili ihusihwe zaidi ili wanafunzi waweze kutumia istilahi za Kiswahili na kuzihusisha na utamaduni wake. Wanafunzi nao wahimizwe kujiepusha na tafsiri za moja kwa moja kutoka Kiingereza hadi Kiswahili.

### Maoni mengine

Ningependa kusisitiza kwamba wanafunzi wapewe nafasi na mazingira mwafaka ya kufanya mazoezi mengi ya mazungumzo wakati wanapoendelea kusoma kozi hii ya Kiswahili.

## Standard level written assignment

**Component grade boundaries**

| **Grade:** | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mark range:** | 0-3 | 4-6 | 7-9 | 10-12 | 13-14 | 15-17 | 18-20 |

### Kiwango na ufaafu wa kazi iliyowasilishwa

Kazi zilizowasilishwa na wanafunzi zilikuwa za kiwango mwafaka na zinazofaa katika kiwango hiki. Wanafunzi walidhihirisha ukomavu wa mawazo na maswala ya kijamii pamoja na ulimwengu unaowazunguka. Mada mbalimbali zinazohusu maudhui ya burudani na kazi, mazingira ya mijini na vijijini, na mtu binafsi na jamii zilishughulikiwa. Kwa jumla mada hizi zinashughulikia binadamu na mazingira yake anamoishi.

### Utendaji wa mtahiniwa dhidi ya kila kigezo

Wanafunzi waliweza kudhihirisha ufasaha wa lugha katika uandishi kwa kujieleza vilivyo. Katika kigezo cha A, wengi waliweza kueleza waziwazi kuhusu mada wanayoishughulikia. Vilevile, wanafunzi wengi waliweza kulinganisha na kulinganua maswala ya utamaduni wao na utamaduni lengwa (wa Kiswahili) katika mada walizozishughulikia. Hata hivyo, changamoto ilikuwa katika kigezo cha C, D na E. Vigezo hivi vinavyohusu tafakari vilionyesha kuwatatiza wanafunzi na kuwafanya wakose alama za juu. Kwa jumla vigezo hivi vitatu vinabeba alama 9 ambapo wanafunzi wanahitajika kueleza bayana tafakari zao kwa kuelekezwa na maswali teule. Ilidhihirika kwamba, wanafunzi wengine walikuwa wanaandika tu sentensi moja au mbili na kukosa kuendeleza maelezo yao kikamilifu. Kwa upande mwingine, Kigezo cha F na G kilishughulikiwa vyema.

### Mapendekezo na mwongozo wa kufundisha watahiniwa wa siku sijazo

Ningependekeza kwamba wanafunzi waweze kuelezwa waziwazi mahitaji ya kigezo cha C, D na E ili wanapoandika insha zao, waweze kuyatilia maanani mahitaji hayo. Ningeomba kwamba kila kipengele au kigezo kinachohusika katika uandishi wa insha hii kielezwe bayana na

wanafunzi waandike insha mbalimbali hata kabla ya insha ya mtihani wa mwisho ili waweze kuboresha uandishi wao.

### Maoni mengine

Ningeomba kwamba wanafunzi waweze kuzoeshwa kuandika mara kwa mara katika mada mbalimbali. Mazoezi ya uandishi yatawakomaza na wawe na uzoefu wa kujieleza katika mitazamo mbalimbali.

## Standard level paper one

### Component grade boundaries

| **Grade:** | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mark range:** | 0-5 | 6-11 | 12-15 | 16-20 | 21-25 | 26-30 | 31-40 |

### Maoni ya jumla

Kwa jumla, karatasi la kwanza limefanywa vizuri. Wanafunzi wameonyesha uelewa wa maswala yanayoshughulikiwa katika matini zilizohusishwa. Majibu mengi yaliyotolewa yalionyesha ufahamu wa vipengele vinavyohusishwa kwa mfano majibu ya “kweli” au “si kweli”, “maneno yenye maana sawa”, “maneno yenye maana kinyume”, kuteua jibu kutokana na yale yaliyotolewa na kadhalika yote yalishughulikiwa vilivyo. Hata hivyo, baadhi ya wanafunzi walionekana kulemewa na maswali yanashughulikia sarufi ya lugha. Wengine walionyesha kubahatisha majibu kwa kuandika maneno mengi katika aya husika ilhali jibu ni maneno machache tu. Kwa kufanya hivi, wanafunzi wanadhihirisha kwamba hawajui hasa majibu. Hii ilikuwa changamoto hasa wakati wa kusahihisha kwa sababu inabidi mtahini apime kama jibu linastahili alama au la kulingana na jinsi lilivyotolewa.

### Sehemu za programu na mtihani zilizooenekana kuwatatiza wanafunzi

Changamoto ya wanafunzi imeonekana katika maswali ya kulinganisha maana, kutafuta kinyume cha maana na yale ya kurejelea na kutafakari. Wanafunzi wengine pia wameonekana kunukuu maneno mengi yasiyohitajika katika maswali ya majibu mafupi.

### Sehemu za programu na mtihani ambazo wanafunzi walionekana kuwa wemejitayarishia vyema

Watahiniwa wameonyesha ukakamavu katika lugha ya Kiswahili. Wamedhihirisha ufahamu wa matini za mtihani na kuweza kujibu maswali vilivyo. Ufanisi mkubwa wa wanafunzi umedhihirika katika maswali ya “kweli” na “si kweli”, maswali ya majibu mafupi na yale na kuteua jibu sahihi kutokana na majibu mengi.

### Uwezo na udhaifu wa watahiniwa kwa maswali binafsi

Watahiniwa wameonyesha ufanisi wa kiwango cha juu katika kushughulikia maswali ya “kweli” na “si kweli”, maswali yanayohitaji kuchagua jibu moja kutokana na majibu mengi na maswali ambayo yanahitaji majibu mafupi. Udhaifu wao umeonekana pale ambapo kuna maswali ya kulinganisha na kutafakari.

### Mapendekezo na mwongozo wa kufundisha watahiniwa wa siku sijazo

Ningependekeza kwamba wanafunzi wapewe maswali mengi ya ufahamu katika mada mbalimbali yanayohusu tafakari ili waweze kudhihirisha uelewa wao katika maswala mbalimbali. Wanafunzi pia washauriwe kujiepusha na kunukuu maneno mengi kutoka kwa matini yanayopotosha jibu linalotarajiwa.

# Standard level paper two

## Component grade boundaries

| **Grade:** | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mark range:** | 0-3 | 4-6 | 7-10 | 11-14 | 15-18 | 19-21 | 22-25 |

### Maoni ya jumla

Karatasi la pili limefanywa vyema kwa jumla. Wanafunzi wengi wameweza kujieleza vyema katika uandishi wa insha za aina mbalimbali kulingana na mahitaji ya mtihani. Sehemu ambazo wanafunzi walionekana kutatizika ni sarufi ya Kiswahili na msamiati. Wakati mwingine mwanafunzi alionekana kupata hoja zote lakini hawezi kujieleza vizuri na hoja hizo zinakosa kujitokeza waziwazi. Hata hivyo, wanafunzi walijitahidi.

### Sehemu za programu na mtihani zilizooenekana kuwatatiza wanafunzi

Wanafunzi wachache walilemewa katika kuwasilisha ujumbe kikamilifu. Wengine walikuwa na changamoto katika matumizi ya lugha. Tanzu walizoziona kuwa na ugumu ni uandishi wa kipeperushi na kutuma hoja kwa ukurasa wa mtandao.

### Sehemu za programu na mtihani ambazo wanafunzi walionekana kuwa wemejitayarishia vyema

Watahiniwa wengi walidhihirisha ukomavu wa mawazo kwa jinsi walivyoweza kujieleza vyema katika tanzu walizoshughulikia. Vigezo vya matumizi ya lugha, ujumbe na sajili vilishughulikiwa vilivyo. Utanzu wa barua pepe na ripoti umeshughulikiwa sana na wanafunzi na wameonyesha kwamba wameumudu vyema.



International Baccalaureate® Baccalauréat International Bachillerato Internacional

## Uwezo na udhaifu wa watahiniwa kwa maswali binafsi

Ufanisi wa watahiniwa ulidhihirika katika uandishi wa barua pepe na ripoti. Utanzu wa mazungumzo pia ulishughulikiwa kwa wastani. Udhaifu ulionekana katika watahiniwa wachache waliojibu maswali ya utanzu wa kipeperushi na kutuma hoja kwa mtandao.

## Mapendekezo na mwongozo wa kufundisha watahiniwa wa siku sijazo

Ningependekeza kwamba wanafunzi wafanye mazoezi mengi ya uandishi wa insha za tanzu mbalimbali kulingana na mahitaji ya IB.


International Baccalaureate® Baccalauréat International Bachillerato Internacional